

# KAMA DHORUBA IMEHARIBU NYUMBA YAKO



Swahili

Dhoruba na mafuriko inaweza kufanya mvunjiko katika vyumba na pia kuwa na uwezekano wa moto, maji au bomba la kuchukulia maji machafu na huduma za gesi kufotanya kazi. Kuna uwezekano pia barabara, uwanja wa ndege au bandari kufungwa na laini ya simu kufotanya kazi.

Utapata kuwa baada ya dhoruba au kufurika utahitaji mahali ya kukaa kighafula, huduma za usaidizi ya hali njema, pesa, chakula au maji.

## KAMA UNA BIMA

- Piga simu haraka iwezekanavyo kwa kampuni ya bima yako kwasababu kampuni mengi inatoa huduma masaa ishirini na nne
- Wanaweza kukupa mahali ya kukaa kwa muda mfupi, chakula na pesa kwa hali ya ugumu ya papo hapo
- Hakikisha nyumba yako iko salama kabla ya kuondoka kwasababu ni jukumu yako kuwa nyumba yako iko salama
- Usijaribu kurekebisha marekebishiye yeyote isipokuwa kama umehitimu, kwasababu hii inaweza kukuweka wewe na familia yako katika hatari au kufanya uharibivu zaidi ambazo haiwezi kuzingatiwa na bima yako
- Kama una maswali ye yeyote kuhusu bima, piga simu Insurance Council of Australia nambari **1300 728 228**

## KAMA HAUNA BIMA

Na familia yako na marafiki hawawezi kukusaidia, wasiliana:

- Department for Child Protection (DCP) nambari **0418 943 835** kwa usaidizi wa mahali ya kukaa kighafula, mavazi, chakula na mahitaji mengine ya lazima
- Department of Housing nambari **1800 093 325** kwa nyumba ya umma au kusaidia na kifungo (bond) ya kukodisha mahali ya kukaa kama unafaulu.

Kama nyumba yako imeharibika vibaya zaidi na unahitaji usaidizi, piga simu SES nambari **132 500**

## MOTO KUPOTEA

- Piga simu Western Power nambari 131 351
- Piga simu Horizon Power nambari 132 351 kama unaishi katika eneo za mkoa (kama hauna uhakika, angalia hesebau yako ya fedha (bill) yako ya mwisho)

## KUSAFISHA

- Anza kusafisha mazunguko ya nyumba yako- rundika vitu ambavyo zimelegalega kama vila matawi na mabaki ya uchafu mbali na mita ya maji, vilango na laini ya simu
- Piga simu kwa serekali ya eneo yako kupata ushauri kuhusu kuondoa takataka ya matawi na vitu vingine kama vile ua ya kuzingira asbestos

*Kwa mawaidha kuhusu jambo la kufanya kabla, wakati na baada ya dhoruba, nenda mtandao [www.fesa.wa.gov.au](http://www.fesa.wa.gov.au)*



Government of **Western Australia**  
**Fire & Emergency Services Authority**

**F E S A**  
Fire & Emergency Services  
Authority of Western Australia